vilivyonukuliwa na mlalamikaji Bw. Nkuruvi havina aina nyingine ya kuuleta mgogoro huu hapa mahakamani zaidi ya njia hizo tatu nilizozieleza hapo juu.

Hoja ya mlalamikaji Bw. Nkuruvi kwamba maadamu kamishna wa kazi sasa ameleta mgogoro mahakamani basi tuunganishe na huu uliopo mahakamani saa hii, hivyo tuendelee kuusikiliza, ni potofu na haikubaliki na Mahakama hii kwani mgogoro huu ulifunguliwa 1998 bila kuleta hapa na kamishna wa kazi na ulipewa Na. 14/98.

Kama kamishna wa kazi kaleta mgogoro kama huu basi labda ulisajiliwa na namba nyingine kwa vyovyote vile ya mwaka 2000 na siyo 1998! si hivyo tu bali pia kwamba mgogoro kama huo hauwezi kuingizwa kwenye jalada hili ambalo tayari lilikuwa limekamilisha taratibu zote za kujibizana kiawali (pleadings) na limepangwa kuanza kusikilizwa kama ilivyo sasa. Kwanza hiyo barua ya kamishna wala haijaingizwa kwenye jalada hili kisahih kabisa. Kama mlalamikaji angetaka kuingiza barua hiyo ya Kamishna wa kazi humu ingebidi labda aombe kwanza kubadili hati yake ya malalamiko kukidhi maendeleo hayo mapya jambo ambalo sidhani mahakama hii ingekubali katika hatua hii.

Utaratibu wa Kisheria uliowekwa kwa ajili ya kuleta mgogoro kwenye mahakama hii usipofuata kwa makini huotesha hisia za kuwepo mazingira ya rishwa au upendeleo kwa upande mmoja jambo ambalo haliwezi kuendekezwa na Mahakama hii. Tangiapo, naye Msomi Bw. Semwaza kama wakili alipaswa alete pingamizi lake la awali mapema zaidi tokea tarehe 11 mwezi Desemba 1998 alipoleta utetezi wake mwajiri hapa mahakamani. Angefanya hivyo mahakama hii ingekuwa imetahadharishwa mapema yeye akiwa ni Afisa wa Mahakama, ili asiundekeze mgogoro na kuuingiza kwenye register yake. Yeye amesubiri hadi mahakama ilipotahadharisha pande zote mbili juu ya uhalali wa mgogoro huu kuwepo hapa 19/4/2000 na tena tarehe 24/4/2000 idipo ukaenda kuleta hoja ya wali mnamo tarehe 30/5/2000 bila hata ya kuomba kwanza kibali cha mahakama hii kufanya hivyo kwani majibizano yote ya awali yalishakuwa yamefanywa na kila upande ukiwa unasubiri kusikilizwa kwa mgogoro huu.

Hata hivyo niliruhusu hoja hii ya awali iliyoletwa bila kufuata utaratibu wa kupata kwanza kibali cha Mahakama hii kwani tayari mahakama hii ilikwishatoa taarifa kwa pande zote kwamba wazungumzie suala hilo na mlalamikaji alikwisha leta utetezi wake kimaandishi kupinga hoja hii ya awali hatua ambayo iliashiria kuwa hana kipingamizi kwa hoja hii ya awali kuleta kwa namna iliyoletwa na Wakili Msomi Bw. Semwaza.

Kwa vyovyote vile mgogoro huu umeletwa kwenye mahakama hii kimakosa kama nilivyoieleza hapo juu. Nautupilia mbali katika ngazi hii ya awali na hauwezi tena kuendelea kusikilizwa kadri ilivyopangwa. Pingamizi la

awali linakubalika na mahakama hii uamuzi huu sasa unakuwa Tuzo na unesomwa leo tarehe 20/7/2000 mbele ya pande zote mbili.

20 Julai, 2000

E. L. K. MWIPOPO, J.  
Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 97

MGOGORO WA KIKAZI NA. 33 WA 2000  
baina ya

DAVID MWAKIKUNGA  
na

CHUO CHA UONGOZI WA MAENDELEO MZUMBE  
UAMUZI

Mwipopo, J.

Mwajiri IDM Institute of Development and Management Mzumbe. Morogoro akiwakilishwa hapa Mahakamani na Bw. D. Bahasha, Afisa Mkuu wa Utumishi na Utawala I (Principal Manpower and Management Officer I) na Wakili wao binafsi (Advocate) Msomi Bw. Massati ameleta hoja za awali kupinga mgogoro huu na kuomba utupiliwe mbali bila ya kusikilizwa. Imedaiwa na kuelezwa na kufafanuliwa mahakamani kwa mdomo na Msomi Bw. Massati Wakili wao kwamba mgogoro huu si chochote na wala hauna lolote la maana la kuweza kuzidi kuendekeza kwenye Mahakama hii ya kazi kwani kwa kifupi tu kama yeye mlalamikaji ni mfanyakazi basi anechelewa na anabanwa na kiina cha muda kilichowekwa cha kuleta migogoro kazi mahakamani chini ya vifungu vya 4 na 5 vya Sheria ya kazi. Imedaiwa kwamba yeye Bw. David Mwakikunga hakufungua mgogoro wake kwenye Tawi la Chama cha Wafanyakazi kazini pake IDM. ndani ya siku 7 wala hakuupeleka mgogoro wake kwa Katibu wa Wilaya wa Chama chao cha Wafanyakazi au kwa Afisa kazi wa Wilaya ndani ya siku 14, wala Afisa wa kazi wa Wilaya hakuusuluhisha mgogoro huu na kuupeleka kwa Kamishna wa Kazi ndani ya siku 30 na hatimaye hata Kamishna wa Kazi mwenyewe hakuusuluhisha na kuuleta mgogoro huu kwenye Mahakama hii chini ya kifungu cha 6 cha Sheria ya Mahakama ya Kazi ya mwaka 1967 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 3 ya mwaka 1990 na Sheria Na. 2 ya mwaka 1993, ndani ya siku 21.

Hoja ya pili ya Mwajiri IDM imeelezwa na Msomi Wakili Bw. Massati kwamba iwapo mlalamikaji ni kiongozi ambaye hapaswi kuwa mwanachama wa chama cha wafanyakazi basi alipaswa apeleke mgogoro wake kwa Afisa Leba wa wilaya ndani ya siku 14 naye Afisa Leba wa Wilaya alipaswa ausuluhisha mgogoro huo ndani ya siku 30 na akishindwa kuwasuluhisha kati ya mfanyakazi kiongozi na Mwajiri wake basi angepaswa aupeleke kwa Kamishna wa Kazi ndani ya siku 30 hizo. Hatimaye naye Kamishna ingepaswa awasuluhisha na akishindwa naye aulete mgogoro kwenye mahakama hii ndani ya siku 21 tokea aletewe mgogoro huo.

Hoja za kwanza na pili za hapo juu Msomi Bw. Massati (Wakili) aliziunganisha na kuzifanya ziwe hoja moja tu ya kwanza. Lakini mimi kwa ajili ya kuandika uamuzi huu nitazitenganisha na kuzifanya ziwe ni hoja mbili tofauti kwani hoja ya kwanza inahusu mambo mawili tofauti ya mfanyakazi aliye mwanachama wa chama cha wafanyakazi aliyeungwa mkono na kutetewa na chama chake cha tawini au aliyekataliwa kutetewa na Tawi lake la mahali pa kazi na kumbe basi hoja yangu ya pili inahusu mfanyakazi aliye kiongozi ambaye havezi kuwa mwanachama wa chama cha wafanyakazi.

Hoja ya tatu kwa madhumuni ya uamuzi huu (ambayo ni hoja ya Pili kwa upande wa Msomi Bw. Masatti/Wakili) ni kwamba iwapo Kamishna wa Kazi alitaka kuuleta mgogoro huu kwenye Mahakama hii chini ya kifungu cha 8 cha sheria hiyo ya Mahakama ya Kazi kama alivyofanya kwenye mgogoro huu basi mlalamikaji alipaswa kuleta Certificate ya Afisa Kazi kuonyesha kuwa yeye ni kiongozi kwenye management ya Mwajiri Chini ya Kifungu cha 10 cha Sheria hiyo hiyo ya Mahakama ya Kazi jambo ambalo hakulifanya kwenye mgogoro huu.

Hoja ya nne kwenye uamuzi huu (ambao ni hoja ya awali ya tatu ya Msomi Wakili Bw. Massati) ni kwamba mlalamikaji hana haki ya kuubeza na kuupinga mkataba wa hiari kati ya Chama cha Wafanyakazi kiitwacho RAAWU (Research and Academic Workers Union) na Mwajiri mbele ya Mahakama hii kwa sababu yeye si mwakilishi halali wa RAAWU kwa hiyo hana Locus standi kwenye mahakama hii. Wakili Msomi Bw. Massati alitilia nguvu hoja hii kwamba ndio msimamo wa kisheria ambao Mahakama hii haina budi kuufuata kwa kunukuu kesi ya Bhogal vs International Computer (EA) Ltd 1972 EA 55 iliyoamuliwa kuwa vipengere vya TUZO ya Mahakama ya Kazi vinawabana wale tu walioingia kwenye (Washiriki) Mkataba (waliotiliana sahihi au kukubaliana kwenye mkataba huo (An Industrial Court Award is binding only between the parties to the award).

Kwa kufafanua zaidi hoja hii Wakili Msomi Bw. Massati aliipanua kwanba hata kama mlalamikaji aliguswa na Mkataba huo kwa kuufaidi matunda yake au kudhurika na vipengere vyake kwa njia ya kuachishwa kazi na kulipwa marupurupu chini ya TUZO ya Mahakama hii ya Mkataba wa Hiari kati ya Mwajiri/IDM na chama cha Wafanyakazi RAAWU bado hana haki ya kuushtakia mkataba huo mahakamani kwa kunukuu kitabu cha Sheria cha Mikataba Africa Mashariki Toleo la 5 kilichoandikwa na R. W. Hodgkin ukurasa wa 231 kinachoelekeza kwamba mtu asiye kwenye mkataba hawezi kufaidi chochote kilichomo mkatabani. Kama atafaidi lolote kutokana na mkataba huo bado hawezi kushtaki mahakamani kwa kuutumia mkataba huo ambao si wake. (Law of Contract in East Africa 1975 Edition, by R. W. Hodgkin at p. 231: "who is not a party to a contract between x and y cannot derive a benefit of it. If he is to benefit from it he cannot sue based on the XY contract".)

Hoja ya tano ya uamuzi huu (ambayo ni hoja ya 4 ya Wakili Msomi Bw. Massati) ni kuwa kwa vile Mkataba wa Hiari

kati ya RAAWU na IDM ulipitishwa na mahakama hii na Mhe. Jaji Bahati J. mnamo tarehe 19/4/96 Mwenyekiti kama alivyokuwa. na ikawa tuzo ya mahakama hii basi haiwezekani tena mahakama hii hii katika ngazi ile ile sawa na ya awali wakati Tuzo inatolewa kuirudia na kuifanyia masahihisho ya kuiponda Tuzo hiyo ya Mkataba wa Hiari bila kwanza kuipeleka mbele kwenye ngazi ya juu zaidi kwa njia ya marejeo (Revision) ambapo Mahakama hii itakaa mahakama kamili (Full Bench) ya Mwenyekiti. Manaibu Wenyeviti wawili na waungwana Wazee wa Mahakama Wawili (jumla watano).

Kwa sababu zote hizo hapo juu kama nilivyozifupisha. Msomi Bw. Massati Wakili. ameomba kwa niaba ya Mwajiri IDM. mgogoro huu kwa ujumla wake utupiliwe mbali sasa na daima.

Mlalamikaji Bw. David Mwakikunga ambaye alikuwa amejiririwa kama kama Afisa Usafiri Mwandamizi (Senior Transport Officer) na hatimaye kupewa kazi ya Dereva Mwandamizi ameleta majibu kupinga hoja zote tano za awali kwa maandishi na pia kwa maelezo ya ndomo na ufafanuzi alioufanya hapa mahakamani ambao kwa kifupi ni kwamba mgogoro huu haujapitwa na wakati kwani mgogoro huu haukuletwa chini ya vifungu vya 4, 5 na 6 bali umeletwa chini ya Kifungu cha 8 cha Sheria ya Mahakama ya Kazi kama ulivyorekebisha na kwa hiyo amedai kuwa muda wa kuuleta mgogoro huu kwenye Mahakama hii ni ndani ya miaka 6 chini ya Sheria ya Kikomo cha muda ya mwaka 1971 Jedwali la kwanza aya ya 7 (Law of Limitation Act 1971 1st schedule para 7) kwani yeye ameleta mgogoro huu kuhusiana na mkataba wake wa kazi wa ajira ambao ulisitishwa na mwajiri isivyo halali.

Kwa upande wa hoja ya tatu ya kuleta hati ya Afisa Leba kuonyesha kuwa yuko kwenye utawala (management) ya IDM Bw. David Mwakikunga amejibu kuwa chini ya Kifungu cha 8 cha Sheria hiyo ambacho ndicho Kamishna wa Kaz amekitumia katika kuuleta mgogoro huu hapa haihitaj kuwepo hiyo certificate ya Labour Officer kuwa yuko kwenye Management. Ameongeza kwamba Certificate ya Afisa Kazi inavyohitajika kwenye kifungu cha 10 hutolewa na Afisa wa Kazi na siyo yeye na kwamba kwa vyovyote kilichotolewa kama ipasavyo kadri alivyokionyesha ana kwa ana mahakamani na akaomba kitolewe kama kielelezo na kwamba afisa Kazi aliyetajwa kwenye Certificate hiyo kwa jina la Ilembu mahakama ikipenda imwite mahakamani kuja kuthibitisha kama aliitoe Certificate hiyo au la.

Kwa upande wa hoja ya nne ya yeye kutokuwa na locus standi kwenye mahakama hii mlalamikaji Bw. David Mwakikunga amepinga hoja hiyo kwamba yeye ni mshiriki wa Mkataba wa Hiari uliotiwa sahihi na kutolewa tuzo hapa mahakamani kwa njia ya yeye kama mfanyakazi kuwasilishwa na wale waliotia mkataba huo. Alifafanua zaidi kwamba pia amefaidi matunda ya kimkataba huo kwani alilipwa mafao yake kupitia mkataba huo mafao ambayo si kamilifu kwani hakupewa fedha za kutosha kumsafirisha yeye na familia yake na mizigo hadi kijijini kwake - Kilasilo,

Kyela. Mbeya kupitia. Dar es Salaam kwa train 1st Class TAZARA hadi Mbeya kwa gari (basi) hadi kijijini kwake. Posho ya njiani pia alisema alipunjwa.

Kuhusu hoja hii ya nne ya kutokuwa na locus standi kwenye mahakama hii Bw. Davidi Mwakikunga alileta majibu mbadala wa majibu yake kwamba yeye ni mshiriki wa mkataba wa hiari kwa kueleza mahakama hii kuwa yeye ameleta mgogoro huu si kwa kutegemea Mkataba huo wa hiari ulioandikishwa na kuwa tuzo mbele ya mahakama hii bali kwa kutegemea sera ya serikali Kuu ya kupunguza wafanyakazi fulani fulani ambao na yeye aliangukia humo na kwa vyovyote mkataba waliotumia waajiri wake IDM kumpunguza kazi si huo wa Tuzo ya mahakama hii bali ni mkataba mwingine ambao wameuacha kuutumia kwenye mgogoro huu. Pia Bw. David Mwakikunga aliongeza maelezo zaidi kuwa barua ya kumpunguza kazi itamka bayana kuwa alikuwa anapunguzwa kazi kwa msingi wa sera ya Serikali Kuu.

Kwenye hoja ya tano Bw. David Mwakikunga alijitetea kuwa suala lililopo hapa mahakamani si kuipitia tena mkataba huo na kuuandikisha upya kwa mara ya pili bali ni kuuchunguza kama kulikuwa na udanganyifu katika kuuleta kwenye mahakama hii kwa njia ya "Fraud" au "misrepresentation" kwa hiyo ni sahihi kwa mahakama hii kukaa kama ilivyo na kuusikiliza mgogoro huu.

Wakili Msomi Bw. Massati alijibu baadhi ya hoja za utetezi za mlalamikaji kwa kupinga kutolewa kielelezo cha Certificate ya Labour Officer aliyoiyonesha mahakamani kwa mara ya kwanza kwenye kikao hiki kwani alisema haikuwa na maoni yoyote ya Labour Officer. Pia Msomi Bw. Massati amenukuu kesi ya JUWATA vs KIUTA (Full bench court of Appeal) (1988) TLR 146 ili kuonyesha kuwa kikomo cha muda kwa mgogoro ya kazi chini ya Sheria ya Mahakama ya Kazi haijatajwa bayana bila kuacha mashaka yoyote na ni lazima jangukie kwenye kikomo cha muda cha kesi za madai ya kawaida chini ya Sheria ya Mikataba (Law of Contract) ili Sheria ya kikomo cha muda ya mwaka 1971 iweze kutumika. Na kwa vyovyote vile Msomi Bw. Massati aliongeza kuwa kama angetaka kushtaki kwa kuvunja mkataba wa Kazi wa Ajira "for breach of the employment contract" basi angefungua kwenye mahakama ya kawaida chini ya sheria ya mikataba au tortious liability n.k. madai ambayo hayawezi kuletwa kwenye mahakama ya Kazi na wala hakuleta mgogoro huu kwa msingi huo.

Msomi Bw. Massati aliendelea kufafanua kuwa iwapo vifungu vya 4 na 5 vya Sheria ya Mahakama ya Kazi havikufuatwa basi hata Kamishna wa Kazi hawezi tena kukitumia kifungu cha 8 cha sheria hiyo katika kuuleta mgogoro wa uchunguzi kwenye mahakama hii na kwamba katika kutumia kifungu cha 8 cha sheria hiyo lazima ihusu tu kiongozi kwenye management ya mwajiri na si mfanyakazi aliye mwanachama wa Chama cha Wafanyakazi kama RAAWU n. k.

Waungwana wazee wa Mahakama wote wawili wametoa maoni yao yanayolingana kwamba mgogoro huu utupiliwe mbali katika ngazi hii. Muungwana Bw. Sultani ametoa sababu ya kuutupilia mbali mgogoro huu kwamba mlalamikaji hana Certificate ya Labour Officer kuonyesha yeye yuko kwenye uongozi na hati aliyoleta hapa mahakamani na kutaka kuitoa kama kielelezo amesema inaelekea imegushiwa tu na si halali. Muungwana Bw. Shing'enda ameunga mkono maoni ya mwaungwana mwenzake na kuongezea kuwa mlalamikaji ashauriwe na Mahakama hii kurudi kwa mwajiri ili akatoe hesabu ya mafao yake ya kupunguzwa kazi ambayo anaona amepunjiwa ili Mwajiri afikirie kama ni kweli alipunjiwa basi aweze kulipwa nyongeza ya mafao hayo na Mwajiri wake.

Kama kuna mahali ambapo methali ya Kiswahili ya akili nyingi huondoa maarifa inaweza kutumika mia kwa mia basi ni kwenye mgogoro huu katika hoja hizi za awali. Kama alivyojisifu mwenyewe mlalamikaji ameshakwenda kwenye mahakama nyingi sana na ameleta nakala za hukumu za mahakama ya Mkoa ya Morogoro. Mahakama Kuu ya Tanzania na sasa amesema yuko mbioni kwenda Mahakama ya mwisho ya Rufaa ya Tanzania pamoja na kwenye mahakama hii kama ilivyofanya sasa hivi. Ameeleza jinsi, bila shaka labda kutokana na akili zake nyingi na werevu na ujuzi wake mkubwa aliweza kushinda hata kwenye mahakama Kuu (Ni kweli alishinda kwenye hukumu ya rufaa ya Mahakama Kuu (High Court (DSM) Civil Appeal No. 148/96: Davidi Mwakikunga vs Governing Body IDM Mzumbe. By Hon. Bubeshi, J.) na anaweza kushinda hata kwenye mgogoro huu mbele ya Mahakama hii na akaomba mgogoro huu uendelee kusikilizwa katika Vipengere vyote. Sina budi kumsifu mlalamikaji Bw. David Mwakikunga kwamba pamoja na kwamba yeye alikuwa Senior Transport Officer tu ambaye mwajiri wake alimpangia kesi ya Senior Driver kabla ya kupunguzwa na pamoja na kutokuwa na Wakili lakini ameweza kujieleza vizuri sana na kukabili hoja zote 5 za uamuzi huu barabara na kwa makini kana kwamba ni mwanasheria mzoefu. Mlalamikaji si mtu ambaye anaweza kudanganyika kirahisi au kukalia haki yake kwa kutokujua sheria au utaratibu unaopaswa kufuatwa katika kukidhi madai na haki zake za kupunguzwa kazi.

Papo hapo mahakama hii kwenye uamuzi huu itajihusisha na mgogoro huu katika ngazi hii ya pingamizi za awali kwenye masuala hayo matano niliyoeleza hapa juu. Juu ya hoja ya kwanza na ya pili kwamba mlalamikaji hakupeleka mgogoro wake kwenye tawi lake la RAAWU Mzumbe IDM Morogoro ndani ya siku 7 na Tawi kupeleka kwa Labour Office ndani ya siku 14 ni wazi kabisa kuwa mlalamikaji Bw. David Mwakikunga hakufanya hivyo labda kwa vile alitaka kulishughulikia kwenye mahakama ya kawaida. (District Court) aliridhika na kupunguzwa kazi, alijiona yeye ni kiongozi na si mfanyakazi wa kawaida n.k. Kwa vile alikuwa Senior Transport Officer mwenye dhamana ya Senior Driver wakati anapunguzwa kazi na madereva walio wengi kwenye mashirika ya Umma wamo kwenye operational service n. k. inawezekana yeye hakuwa kiongozi na

alipaswa aripoti mgogoro wake kwenye tawi lake la RAAWU au kama si mwanachama alitakiwa atoe ripoti ya mgogoro huu kwa District Secretary wa RAAWU Morogoro ndani ya siku 7 na 14 hadi mgogoro huo ufikie siku 14 nyingine tena baada ya hapo. Vile vile kama yeye alijiona ni kiongozi kwa mwajiri wake basi alitakiwa aupeleke mgogoro wake kwa Bwana Leba wa Wilaya ndani ya siku 14. Mlolongo wa kutotimiza masharti ya vifungu vya 4 na 5 umeendelezwa hadi kwa Afisa Kazi Wilaya hakuupeleka mgogoro huu kwa Kamishna wa Kazi ndani ya siku 30 na Kamishna hakuleta mgogoro huu kwenye Mahakama hii chini ya kifungu cha 6 ndani ya siku 21. Kwa hiyo kwa kutofuata vipengere vya 4, 5 na 6 katika mida iliyowekwa na sheria mgogoro huu unakuwa haupo hapa kihalali na unaweza kutupiliwa mbali.

Kwenye kipengere cha 3 cha hoja za awali juu ya ulazima wa kuwepo kwa Certificate ya Afisa Leba kuonyesha kama mfanyakazi huyu yuko kwenye uongozi wa mwajiri Mahakama hii ilikwisha kataa kupokea Certificate aliyoleta mlalamikaji hapa mahakamani wakati wa kusikiliza hoja hizi za awali kwa sababu zilizoelzwa kwenye uamuzi wa awali wa papo kwa papo kwa kifupi. Kwa vile haikuwa nakala halisi ni kopi tu, kwa vile haikuwa na sahihi yoyote ya Afisa Kazi mhusika, kwa kuwa haikuwa na maoni ya kuonyesha kuwa mlalamikaji ni kiongozi au sio sehemu zinazohusika hazikukatwa, kwa kuwa haikuletwa kwenye pleadings zote za awali na kwa kuwa mahakama isingeliwezakana kumwita mwenye kuiandika fomu hiyo kama alivyoomba mahakama ifanye kwa vile form hiyo ilikuwa haina sahihi yeyote ili tujue tumwite nani aje aitambuaje form isiyo na sahihi yake? Papo hapo sikubaliani na Msomi Massati kwamba kwa kutumia kifungu cha 8 lazima kamishna wa Kazi abanwe na vifungu vya 4 na 5 na 6 vya sheria hiyo kuhusu muda wa kuleta mgogoro huu hapa. Kamishna wa Kazi ana uhuru wa uwezo chini ya kifungu cha 8 kuleta mgogoro wa uchunguzi hata kama mgogoro huo uko nje ya mida iliyowekwa kwenye vifungu vya 4, 5 na 6 na hata kama haukupitia ngazi hizo za Tawi la Chama cha wafanyakazi, Wilayani kwa chama au kwa Afisa Leba wa Wilaya. Pia sikubaliani na Msomi Bw. Massati kwamba lazima kila Kamishna wa Kazi anapoleta mgogoro wa uchunguzi chini ya kifungu cha 8 pia kifungu cha 10 kifuatwe kwamba mgogoro huu lazima uwahusu tu kiongozi na huyo kiongozi awe na Certificate ya Labour Officer. Kamishna wa Kazi anaweza kuleta mgogoro chini ya kifungu cha 8 hata kama unamhusu Mwanachama wa chama cha Wafanyakazi au asiye mwanachama na si kiongozi wake mwajiri na hata kama ni Chama chenye yeye cha wafanyakazi yaani kwa mfano kama RAAWU yenyewe ingekuwa ndiyo iliyompelekea Kamishna wa Kazi mgogoro huu bado kifungu cha 8 kingeweza kutumikia bila haja ya kufuta matakwa na kukitumia tena kifungu cha 10 cha sheria hiyo.

Kwa upande wa mgogoro huu maadamu mlalamikaji amesema ni kiongozi na ameshindwa kuleta Certificate ya Afisa Leba basi kifungu cha 8 kinambana kikamilifu yeye pekee. Kama Kamishna kwa Kazi asingechukua mgogoro huu kwa uchunguzi, basi mlalamikaji asingeweza kuuendeleza mgogoro huu kihalali kwenye mahakama hii.

Kuhusu hoja ya nne kwa mlalamikaji kudai kuwa yeye ni mshiriki wa Mkataba wa Hiari wenye Tuzo ya Mahakama hii kwa vile ni mfanyakazi aliyewakilishwa na tawi la RAAWU hakumsaidia kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Mikataba Cap 434 kifungu cha 2 (d) kadri ya ufafanuzi wake Mwandishi R. W. Hodgkin kwenye kitabu chake cha Law of contract in East Africa P. 34 na pia chini ya uamuzi wa Mahakama kuu ya Kenya kwenye kesi ya *Bhojal vs International Computers (EA) Ltd (1972) E. A. 55* uamuzi ambao ni sawa kabisa na msimamo wa sheria ya nchi hii na Mahakama hii kuhusu suala hili. Ingawaje mlalamikaji amefaidi mafao ya Mkataba wa Kazi wenye TUZO ya Mahakama hii alipopunguzwa chini yake bado yeye si mshiriki wa mkataba huo uliotiwa sahihi kati ya RAAWU na I.D.M. tu na si yeye binafsi.

Vile vile maelezo mbadala kuwa yeye hahusiki na tuzo ya mkataba huu kwa vile alipunguzwa kwa mujibu wa sera ya Serikali ni upuuzi mtupu kwani yeye si mtumishi wa Serikali kuu bali ni wa I.D.M. inayojitegemea kijira na inaweza kushtaki na kushtakiwa na ndiyo maana kwenye kesi ya Mahakama kuu niliyoitaja hapo juu aliifungulia Governing Board ya I.D.M. Mzumbe na siyo Attorney General au Katibu Mkuu Utumishi etc. Mashtaka yake ya mgogoro huu hayakuletwa kwa njia ya kubeza sera ya Serikali au kuunga au kutaka ukazaji wa sera za Serikali utekelezwe. Si hiyo tu, kama alivyoeleza Msomi Bw. Massati kiusahili ni kutokana na sera ya Serikali ya upunguzaji wafanyakazi ndiyo maana mkataba wa hiari ulioandikishwa na kupata Tuzo ya Mahakama ulitengenezwa kiutekelezaji. Kwa hiyo nakubali hoja kuwa mlalamikaji hana Locus standi ya kuupinga mkataba wa Hiari wenye Tuzo kwenye Mahakama hii kwa njia ya mgogoro huu. Awaachie RAAWU wafanye hivyo kama wangependa na si yeye binafsi.

Hoja ya Tano ni ya wazi kuwa Mahakama hii haiwezi kukaa kuitengua Tuzo ya Mkataba wa Hiari aliyandikisha Mhe. Jaji Bahati (Mwenyekiti) kama ilivyoittoa tarehe 19/4/96 ikikaa kama ilivyo sasa kwenye mgogoro huu ila labda kama itakuwa kwa njia ya Revision with full Bench ya Mahakama hii hatua ambayo siyo ilioombwa au kufikiwa kwenye mgogoro huu.

Kuna hoja nyingine ya Msomi Bw. Massati kwamba mlalamikaji afungue kesi ya madai ya Breach of contract na tort kwenye Mahakama za kawaida na sio kwenye Mahakama hii ya kazi ili aweze kufaidi time limit ya miaka 6 ya kufufua kesi ya madai chini ya Law of Limitation Act 1971 n.k. kwanza kabisa mlalamikaji hawezi kwenda kufanya hivyo sasa kwani Sheria ya madai au C.P.C. zimembana asifanye hivyo sasa kwa sababu alishafungua kesi za madai kwenye mahakama za kawaida kwa kukataa mkataba wote

wa kazi jambo ambalo liliongelewa hata kwenye hukumu ya Mahakama Kuu niliyonukuu hapo juu. Madai yote yanayohusu Mkataba wa kazi na kupunguzwa kwa kimkataba au kiutaratibu alipaswa ayaingize kwenye kesi hizo. Kama hakufanya basi alikalia haki yake.

Kwa upande mwingine mahakama hii imekwishotoa uamuzi katika ngazi ya full Bench under Revision kwenye

mgogoro wa Marejeo Na. 12/98 Abdallah O. Mkunga v. Tanzania Bottlers Ltd. (Unreported) kwamba ingawaje Kamishna wa kazi habanwi na vikomo vya muda vilivyowekwa kwenye vifungu vya 4, 5 na 6 vya sheria ya Mahakama ya Kazi bado amebanwa na Sheria ya kikomo cha muda ya mwaka 1971 chini ya Jedwali la kwanza aya ya 7 kwamba lazima aulete mgogoro wa uchunguzi kwenye mahakama hii ndani ya miaka 6 tokea ajira ya Mfanyakazi huyo isitishwe. Katika kesi hiyo Kamishna wa kazi alileta mgogoro kwa uchunguzi chini ya kifungu 8 baada ya karibu miaka 8 kupita. Uamuzi wa kesi hiyo imejazia na kuondoa wasiwasi ulioelezwa na Mahakama ya Rufaa katika kesi ya CTTU vs KIUTA (1988) TLR 146 kwamba haiwezekani migogoro ya kikazi ikaendelezwa kila mfanyakazi anapokurupuka kufanya hivyo.

Ndiyo maana pale mwanzoni nilitamka kwamba akili nyingi za mlalamikaji zimemwondolea maarifa madogo madogo tu ya kuushughulikia mgogoro wake huu na sasa nalazimika kukubaliana na Msomi Bw. Massati, na waungwana wote wawili wa mahakama hii kwamba mgogoro huu utupiliwe mbali kiawali na unatupiliwa mbali kiawali na daima yaani bila kuagiza kuwa ufunguliwe tena kwa kufuata taratibu zilizo ndani ya sheria. Uamuzi nimeutoa mbele ya pande zote leo 21/7/2000 na sasa ni tuzo ya Mahakama hii.

B. L. K. MWIPOPO, J.  
Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 98

USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Mwanzo Ukonga)  
*Maombi ya barua za Usimamizi wa Mirathi ya*  
*Patrick Kipambe*

na

Adolfina Chitamo-Muombaji

S. S. M. 1984 NYONGEZA  
(ya 5 Kanuni ya 2)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 20 Mei, 2001 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Tarehe 20 Februari, 2001

Sahihi ya Hakim.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 99

DEED POLL ON CHANGE OF NAME

BY THIS DEED, I, DORAH TABU HAULE of C/O P.O. BOX 10336, Dar es Salaam do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former names TABU DORAH HAULE and in lieu thereof do assume and adopt this 15<sup>th</sup> day of February, 2001 the name of DORAH TABU HAULE.

AND IN PURSUANCE of such change of name as aforesaid, I HEREBY DECLARE that I shall at all times hereafter in all records, deeds and instruments in writing and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever, use and sign the name of DORAH TABU HAULE as my name in lieu of the said name of TABU DORAH HAULE Renounced as aforesaid.

AND I HEREBY AUTHORISE and request all persons to designate and address me in the name of DORAH TABU HAULE only.

In Witness Whereof I have hereunto set my hand this 15<sup>th</sup> day of February, 2001.

SIGNED and DELIVERED by the said  
DORAH TABU HAULE who has been  
identified to me by MR. TIMOTHY HAULE  
the latter being known to me personally in  
my presence this 15th day of February, 2001

DEPONENT

BEFORE ME:

*Commissioner for Oaths* 